

## **KITENGO CHA UFUGAJI NYUKI**

### **UTANGULIZI**

Wilaya ya Bukombe ni miongoni mwa wilaya inayopatikana mkoani Geita. Wakazi wa wilaya ya Bukombe kwa asili wanajishughulisha na ufugaji wa nyuki hata kabla ya Uhuru hii ni kutokana na kuwa na Manzuki nzuri na yakutosha. Wilaya imezungukwa na misitu ya Asili ambayo ni Msitu wa Ushirombo, Msitu wa Bukombe/Mbongwe, Msitu wa Kahama/Biharamulo pamoja na Hifadhi wa Wanyamapori Kigosi/Myovosi. Maeneo haya yote yana misitu ya miombo hivyo kufanya kuwa na Manzuki nzuri na yakuvutia kwa nyuki. Kutokana na hali hiyo imeifanya Wilaya Bukombe kuwa moja ya wilaya chache zinazozalisha asali mahuluku na kwa wingi nchini Tanzania.

### **SHUGHULI ZA KITENGO**

- ✓ Kuhamasisha njia bora za ufugaji nyuki ndani ya Wilaya.
- ✓ Kuhamasisha jamii Kuhusu ubora na usalama wa mazao ya nyuki.
- ✓ Kuimarisha uwezo wa jamii katika kusimamia na matumizi ya sheria, kanuni na sera za ufugaji nyuki.
- ✓ Kutoa mafunzo ya ufugaji nyuki bora wa kisasa kwa vikundi vya ufugaji nyuki, taasisi na watu binafsi.
- ✓ Kukusanya takwimu sahihi za wafugaji Nyuki pamoja na uzalishaji wa mazao ya Nyuki

- ✓ Kushirikiana na taasisi mbalimbali za serikali na zisizo za serikali kutoa Elimu za Ufugaji Nyuki wa Kisasa
- ✓ Kusimamia na kuwapa elimu wafanyabiashara na wadau wa mazao ya Nyuki juu ya ubora wa mazao ya Nyuki

## **UZALISHAJI WA MAZAO YA NYUKI**

Wilaya ina shirikisho la vikundi wafugaji Nyuki lenye Vikundi vya wafugaji nyuki vipatavyo ishirini na tano na SACCOS tatu za wafuga Nyuki lenye jumla ya wafugaji nyuki 2123 ambao wanazalisha mazao ya nyuki (asali na nta), kama inavyooneshwa kwenye jedwali lifuatalo;

### **Takwimu za ufugaji nyuki wilayani Bukombe kwa mwaka 2015/16 hadi 2017/18**

<b>Mwaka</b>	<b>Idadi ya Vikundi</b>	<b>Idadi ya wafugaji</b>	<b>Idadi ya mizinga</b>		<b>Mavuno (Tani)</b>		<b>Fedha iliyopatikana (Tsh) '000</b>	
			Kisasa	Kienyeji	Asali	Nta	Asali	Nta
2015/16	20	795	1221	364661	295	18	146,359	146,064,
2016/17	21	1745	1481	170458	377	10	887,065	76,678
2017/18	25	2123	2083	169575	672	43	1,792,013	395,883

*Chanzo: Ofisi ya Ufugaji Nyuki 2018*

Kwa mwaka 2017/18 Wilaya ya Bukombe inategemea kuuza tani 420 za asali nje ya nchi na Tanzania na kiasi cha tani 252 ndani ya nchi .

Kutokana na mauzo haya Halmashauri ya wilaya inategemea kukusanya zaidi ya shilingi za kitanzania milioni arobaini (40,000,000/=) ambazo ni ushuru wa asali na nta.

## **MAFANIKIO SEKTA YA UFUGAJI NYUKI**

- ✓ Kuanzishwa kwa shirikisho la wafugaji nyuki wilayani Bukombe
- ✓ Shirikisho limenunua eneo kwa ajili ya ujenzi wa ghala la kukusanya, kuchakata na kuuza mazao ya nyuki
- ✓ Kuongezeka kwa idadi ya wafugaji nyuki na idadi ya mizinga ya kisasa
- ✓ Uelewa wa ufugaji nyuki kwa wananchi umeongezeka

## **CHANGAMOTO ZA SEKTA YA UFUGAJI NYUKI**

- ✓ Uvamizi wa misitu kwa shughuli za kibinadamu kama vile kilimo, ufugaji, uchimbaji wa madini, ukataji wa miti kwa ajili ya mkaa, mbao na nguzo.
- ✓ Kutokuwepo na kituo maalum cha kukusanya na kuchakata na kuuza mazao ya nyuki
- ✓ Upungufu wa watumishi:
- ✓ Ufinyu wa bajeti na upatikanaji wa fedha za kusimamia raslimali misitu na ufuutiliaji wa shughuli za ufugaji nyuki
- ✓ Mabadiliko ya tabia nchi
- ✓ Upatikanaji ya zana za kisasa za ufugaji nyuki na uchakataji wa mazao ya nyuki

- ✓ Uelewa duni wa wafugaji nyuki juu ya mbinu bora za ufugaji nyuki wa kisasa na uchakataji wa mazao ya nyuki

## **MIKAKATI YA KUBORESHA SEKTA YA UFUGAJI NYUKI WILAYANI**

- ✓ Kuboresha vikundi vilivyopo kwa kuviunda upya na kuvisajili ili kurahisisha utoaji wa huduma inayohitajika.
- ✓ Kulasimisha shirikisho la vikundi vyta wafugaji nyuki ili kurahisisha utoaji wa taarifa na huduma mbalimbali kwa wafugaji
- ✓ Kuhakikisha uwepo wa kituo maalum cha kukusanya, kuchakata na kuuzia mazao ya nyuki, na upatikanaji wa vifaa vyta ufugaji nyuki wa kisasa ndani ya wilaya.
- ✓ Elimu endelevu kwa wafugaji nyuki ni muhimu ili kuongeza uhifadhi wa misitu na kuongeza ubora na wingi wa mazao ya nyuki.

## **MAWASILIANO**

### **1. Mkuu wa Kitengo**

**Dafrosa Shayo**

**Namba ya simu: +255620248003/+255759083127**

**Email: [dafshayo@gmail.com](mailto:dafshayo@gmail.com)**

### **2. Afisa Ufugaji Nyuki**

**Kusekwa B. Maisha**

**Namba ya simu: +255753723109**

**Email: maishakb2006@gmail.com**